# UFAHAMU

# WA

# MAONO

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha UFAHAMU WA MAONO. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk biblia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

UFAHAMU WA MAONO

1.Maono ni nini?………………………………………………….

2. Neno la Mungu (Upako)……………………………………..

3. Giza…………………………………………………………….

4. Malaika…………………………………………………………

5. Nyoka…………………………………………………………..

6.Damu ya Yesu……………………………………………….

7.Mlemavu……………………………………………………….

8. Jengo la Kanisa……………………………………………..

9. Nyumba,suti,shati na gari……………………………………

10.Mtu analia kwa kutaka kutaka msaada mtu, Mimba,Maji ………………………………………………………..

13.Sauti ya Mungu………………………………………………

14.Kuokoka………………………………………………………

15. Mwisho………………………………………………………

# 1. MAONO NI NINI?

**Maono** ni kuoneshwa na Roho mtakatifu mambo ya baadaye yatokayo kwa Yesu au kupashwa habari za baadaye kwa kuoneshwa na roho mtakatifu ukiwa umelala usiku au ukiwa macho yaani hujalala usingizi pengine nyakati za mchana mf: ktk ibada, maombi, unatafakari biblia,umepumzika n.k

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka uyastaajabilie madiliko kama ya kuona maono au kuota ndoto za kweli hutokea ndani yako kama njia ya roho mtakatifu kufikisha ujumbe wa mungu kwako na kuwasiliana nawe. Wakati mwingine mungu hutumia maono kujibu maombi yako.

**Matendo 2.17**

"Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona **maono;** na wazee wenu wataota **ndoto.** "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka pengine ni mwalimu wa hesabu ktk shule za kimataifa kama kijana ukijaa roho mtakatifu mungu uweza kutumia maono kuwasiliana nawa au kama mzee hutumia ndoto kuwasiliana nawe kukupasha mambo ya baadaye yatokayo kwa Yesu.

**Yoh 16.13**

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo **atawapasha** habari yake. "

Maono yakikupata hushudiwa na roho mtakatifu ya kwamba uliloneshwa ni Amina na kweli yaani litakwenda kutukia kweli na pengine limetoka Yesu.

Tangu ulipookoka kama kijana kinachokupata usiku ukilala ni maono si ndoto kama una Roho mtakatifu kadhalika mzee ni ndoto.

# 2.NENO LA MUNGU

Ukiona wazi wazi mfano wa mwana wa mungu akiingia ndani yako ukiwa na vazi la **full suti** yenye mfano wa rangi ya **njano au dhahabu** ujue hilo ni Neno la Mungu huo ni upako ukiokoka. Na wewe ni mtumishi wa mungu. Usifanye uasherati au uzinzi asije akakuharibu.

**Yoh: 1: 1-5**

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule **uzima** ulikuwa **nuru** ya watu.

Nayo **nuru** yang'aa **gizani**, wala **giza** halikuiweza."

Wewe umefanyika nuru utakiwa ukae gizani ulikotwaliwa kwa wenye dhambi uwabadilishe kwa kuwahubiri habari za Yesu. Mengi kuhusu utumishi wako mungu atasema nawe soma biblia na kuomba msaada wa roho mtakatifu naye atakufundisha kweli.Kuanzia siku hiyo jitoe kwa Yesu na utafute marafiki waliokoka wahubiri ,washuhudiaji , wainjilisti achana na marafiki wa zamani tafuta kwenda chuo cha biblia elimu yako ya hekima ya kibinadamu muuzie mungu kama unasoma ukimaliza form four au form six hata umefaulu kwenda vyuo vya kawaida nenda chuo cha biblia au vya wahubiri kama kipo ktk nchi yako. Ishi maisha matakatifu na ya usafi wa moyo tunza upako kwa kutofanya dhambi ya zinaa na zinginezo ziepuke maisha yako yanayotakiwa kuwa na ushuhuda wewe ni mtumishi mkubwa wa mungu.

Jifunze kufunga kumzidi farisayo anayefunga mara mbili kwa Juma wewe zidi hata mara tatu kama tamaa za mwili zinakusumbua u mwenye elimu ya hekima ya kibinadamu wewe jiepushe au punguza matumizi ya vyakula vya protini au mafuta.

## 3. GIZA

Ukiona ktk maono giza zito na unapapasa huoni njia ukiwa umelala na umeokoka ujue nguvu za giza kama uchawi unafuatilia wokovu wako na kama ni mtumishi ujue unaitwa na kuwatoa wenye dhambi gizani unatakiwa ukawahubiri habari njema za yesu mfufuka waokoke.

Pili inawezekana nguvu ya upotevu itakuvaa utapotea njia na kutamani kurudi kule ulikotwaliwa yaani kwenye dhambi kabisa.

Ukioneshwa jambo baya dumu ktk maombi na kuomba rehema na msaada mungu au yesu akuoe na hayo mabaya yasikupate. Usilale ukiona ktk maono jambo baya linakuja mwombe mungu akuepushe ikiwa la kukupa maarifa atakufundisha kwa huyo roho mtakatifu.

Jifunze ktk huu ushuhuda wangu siku moja nilikuwa naumwa malaria kwa mara ya kwanza toka niokoke. Ilikuwa ni usiku kama saa moja au saa mbili usiku nikiwa nimekaa ktk kochi mwili ulikuwa wa moto natetemeka roho mtakatifu akasema nami kwa mawazo swali ni hili niloulizwa na huyo roho wa uzima; ulipokuwa kabla hujaokoka hali kama hii ikupafanya nini? Hali kama hii ningelienda hospitali nilijibu kwa haraka nikaambiwa omba ila cha ajabu siku hiyo nilikuwa ujasiri wa ajabu sina hofu kabisa.Basi usiku ule nikamwomba Yesu aniponye kufika nikalala ,naamka asubuhi homa nimepona kutetemeka kumetoweka malaria imekimbia Yesu ameniponya. Asubuhi hiyo hiyo Roho akanikumbusha maono aliyoniosha usiku juu ya jambo jingine baya lingenipata nalo niliona majipu yanaoka ktk mwili.Siku hiyo nilipata ujasiri nikasema hili siliachi linipate kabla halijanipata ktk mwili nitaomba basi nikaomba Mungu aniepushe majibu na Yesu akafanya hivyo akaniepusha sikuugua kabisa.

Ukioneshwa jambo baya mungu anaweza kukuepusha ukimwomba.

# 4. MALAIKA

Ukiona ktk maono malaika wenye full suti ya njano bila kuona ngozi ya miili yao na hujaokoka ukakutana nao kati ya asubuhi mpaka jioni ufahamu utaokoka hata hawakusema nawe. Ukiokoka mshukuru mungu kwa hilo alilokutendea.

Ukiona ktk maono malaika wenye utaji wa njano umewazunguka ktk umbo la mwili kama la kibinadamu wana asili ya ngozi kama ya Yesu muIsraeli ufahamu wapo kukuhudumia au kukupatia ujumbe utokao kwa Yesu. Mara nyingi malaika wa aina hii Yesu anaweza kukupa neema ya kuwaona ibadani.mfano kukufungua upate kuwa huru na kulitumikia kusudi la mungu au Yesu.

Malaika ni wajumbe au walinzi wanaokaa na watumishi wa mungu waliotumwa au pelekwa na Yesu na kupewa upako na Yesu kwa kazi waliotumwa na mungu baada ya Yesu kukutana nao au mungu kukutana nao.

**Matendo 10**

"...Akaona katika **maono** waziwazi, kama saa tisa ya **mchana, malaika** wa Mungu, akimjia na kumwambia, Kornelio!

Akamtazama sana, akaogopa akasema, Kuna nini, Bwana?
Akamwambia, Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. ...."

Malaika wenye full suti ya njano ni wa nuruni wao hubeba uzima kutoka kwa Yesu au Mungu wapo upande wa Yesu ni wa ufalme wa Mungu. Malaika wa aina hii wengi wapo mbinguni ni wenyeji wa mbinguni. Wachache walioteuliwa hufanya kazi za mungu na watumishi wake aliowatuma au aliowapeleka Yesu na kuwapa huduma kubwa za kanisa ili wahudumie wengi waliokoka.

Ukiona malaika kama hao mshukuru Mungu kwa sadaka & maneno

## 5. NYOKA

Ukiona ktk maono ya usiku unafukuzwa na nyoka ufahamu shetani akutafuta akudanganye ufanye dhambi akupe mabaya ili akutumikise ktk dhambi na kukufanya usimwamini Mungu au Yesu uweze kuacha imani ya wokovu.

Kama ni mtumishi wa Mungu shetani atakuja na mwanamke mwenye VVU kukudanya ukifanya naye uasherati anakuingiza ktk tabu na kuharibu baraka ulizopewa na mungu wako na kukuchewesha ktk utumishi atakunyang'anya muda wa kumtumikia muda wa ujana inapendeza kumtumikia mungu siku za ujana wako kama wale waliokataliwa wenye dhambi huzitoa siku hizo kutumikia dhambi badala ya mungu mfano disko, pombe, cocaine, uasherati, uvutaji wa sigara,rushwa au Ufisadi., mgomvi n.k

**Mwanzo 3**

"Basi **nyoka** alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? …………

Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u **uchi**? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? ………….."

Kama umeoa ufahamu shetani ana mpango wa kumtumia mke kukufanya usitii ulichoagizwa na mungu .

Pia ukiona nyoka ktk maono usiku ukiwa umelala ee mtu wa kimataifa uliyeokoka unafatiliwa au utapambana na uchawi au uganga wa asili kiarabu au zinaa au uasherati. Kesha Yesu akupiganie.

**Kutoka 7: 10 –11**"Basi Musa na Haruni wakaingia kwa Farao, wakafanya vivyo kama Bwana alivyowaambia; Haruni akaibwaga fimbo yake chini mbele ya Farao, mbele ya watumishi wake, ikawa **nyoka.** Ndipo Farao naye akawaita wenye akili na **wachawi;** na hao **waganga** wa **Misri** wakafanya vivyo kwa uganga wao. "

## 6. DAMU YA YESU

Ukiona maono ya damu ya Yesu inakushukia yakijirudia mara tatu ukishuhudia na Roho mtakatifu yatoka kwa Yesu maana yake kama mtumishi wa Yesu itia damu ya Yesu ktk maombi ili ujio wa mungu unapokutembelea upokee upako au Neno la Mungu , ili kutiisha mwili na roho vipate kumtii kristo na kuzuia uharibifu au kutokupatana na upako au ujio wa Neno la mungu na malaika ktk wokovu wako.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ufahamu mambo hayo ukiwa bado u mtoto ulewi upako ni nini? Ujio wa Yesu kwako ni nini ? Ila umepata maono usiku ukiwa umelala kama hapo juu maana inayoufanania ni hii itumie damu ya Yesu kukulinda kwa kuzuia nguvu ya uharibifu inayotaka kupenya ktk eneo lolote la wokovu wako.

Kama changamoto unapitia ujue hiyo njia uzima ya kuvuka ktk changamoto hiyo dumu ktk maombi iitie damu ya Yesu omba Yesu akuondolee dhambi kama ipo umemkosea usiyoifahamu wewe na kuzidi kukutakasa hiyo damu yake.

Chunguza maisha yako kama unatenda kama ulivyoitwa na Yesu au Mungu dumu ktk rehema na kumwambia msaidizi wako akuombee mbele za Baba wa Mbinguni ili uweze kukaa ktk neno la Yesu na Yesu ndani yako sawa jinsi alvyokuokoa na alivyokuita.

**Math 26.27**

“Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki;

kwa maana hii ndiyo **damu** yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa **ondoleo la dhambi.”** Ukiona maono ya damu ya Yesu inashuka kwako Mwambie Roho mtakatifu akuchunguze na kufunua dhambi uliyotenda ya kutubu ili uishi na mungu kwa amani

# 7. MLEMAVU

Ukiona maono una mwombea mlemavu na anaponywa na Yesu usiku ukiwa umelala ukishuhudiwa na roho mtakatifu hilo latoka kwa Yesu na u mtumishi wa Yesu na umeokoka ufahamu kuwa saa ile ulipooneshwa neema na Mungu aliye ndani yako ana uwezo wa kumponya mlemavu wa aina uliyooneshwa au upako ulionao kwa wakati huo unaweza kumhudumia mlemavu wa aina uliyooneshwa. Yesu ni mponyaji.

Ni muhimu ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ukipata maono kwa kuoneshwa na roho mtakatifu dumu ktk maombi ikiwezekana funga ili Yesu akufahamishe maana yake kisha uchukue hatua.

**Math 15.30**

"Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, **vilema**, na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake;

akawaponya; "

Ni Yesu pekee ndiye mwenye uwezo wa kuponya vilema; ukiona unatumiwa na Yesu kuponya vilema ktk maono ya usiku ukiwa umelala ufahamu Yesu ndiye mwenye huo uwezo wa kukutumia kuponya vilema kama ni mtumishi wa Yesu umtafute utamwona ktk utumishi wako akikutumia kuponya walemavu.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka pengine wewe ni mtumishi wa mungu au Yesu na Yesu anataka akuinue uwe mkubwa na uje uwahudumie wenzako wa kimataifa waliokoka au wenye dhambi wapate kuokoka basi upate ufahamu wa maono hayo niliyokuandikia

Yanayoendana kazi ya injili ya Yesu.

Ni utakatifu na usafi wa wokovu wako kama mtumishi wa mungu au wa Yesu ni wa muhimu ktk kutumiwa na Yesu kutenda makuu kama kuponya mlemavu .

# 8. JENGO LA  KANISA

Ukiona Jengo la kanisa na upo ibadani umekaa ufahamu hilo kanisa hutapa nafasi ya kutumikia wenzako ndilo kanisa mungu amekuweka uwe mpole  usiahamie kanisa jingine hilo ndilo Yesu amekulidhia kukaa. Jitoe kumtumikia mungu kwa njia zingine kama matoleo na kudhuhudhuria ibada, maombi, mikesha,semina, tamasha  yote yanayoamriwa na kanisa.

Kama ni mtumishi wa Yesu unajifahamu hilo lisikuumize tafuta huduma iliyo ndani na utimilize inawezekana Yesu anataka akutumie kwenda kuwahubiri wenye dhambi hakikisha ushirika wako na Yesu ni mzuri mwombe Yesu akuoneshe njia uzima ya namna kumtumikia. Ishi maisha matakatifu na Usafi wa moyo epuka uzinzi wasije ukanyang'anywa taji yako na mtu. Uzinzi au uasherati unaweza pelekea Yesu kuchukua upako wake aliokupa.

Kama Huduma yako Roho amekupasha habari ni  mwinjilisti,mtume,nabii,mchungaji,mwalimu,Mtenda miujiza, Mponyaji ,Maongozi, Mhubiri nenda chuo cha utumishi wa mungu na ukasome kama kanisa inacho.Ni vizuri kwenda kwenda kusoma chuo cha huduma husika mfano kama una huduma ya wahubiri kwenda kusoma chuo cha wahubiri.

Huduma za kanisa zote si shida kupata chuo cha utumishi wa Yesu, Isipokuwa wahubiri nchi nyingi vyuo ni vichache vya wahubiri. Kumbuka Mhubiri si mwinjilisti wala si mchungaji. Huduma ni rahisi sana kupata chuo cha uinjilisti au uchungaji sio cha wahubiri. Hivyo ukiitwa mhubiri na Roho mtakatifu ni vizuri kukaa naye chini akufundishe biblia na nafasi yako kisha ujitoe kuwahubiri wenye dhambi waokoke tafuta na vitabu vya wahubiri wa injili uongeze ufahamu wako juu ya hiyo huduma utokao kwa Yesu. Jifunze kwa wahubiri wa injili wengine usisahau kusudi la huduma Yesu anataka ushirikiane naye kwenda kutafuta kilichopotea Watu ambao tangu kuumbwa kwa ulimwengu aliwajua alitaka wafanane naye wanaoishi maisha ya dhambi  wapate kuokoka.

## 9. NYUMBA,SUTI,FLANA NA GARI

Ukiona ktk maono ukiwa umelala umevaa suti nawe u mtu wa kawaida huna suti ufahamu unaenda kukutana mtu aliyeokoka mwenzako atakayejitambulishe mke kwako ktk safari yako ya wokovu. Jiepushe usifanye naye uasherati .

Ukiona ktk maono ukiwa umelala umevaa flana ufahamu uchumba umevunjika kama umeletewa mke aliyejitambulisha mke bila wewe kupata maono kama yeye au kuambiwa na Mungu na kufanya naye uasherati au tendo la ndoa.

Ukiona unapanda ngazi za kwenda orofa ya juu ya ghorofa ghala ile njia unakutwa na ukuta ya kuingia orofa ya juu na unashindwa kupita ufahamu karama kupanda ngazi ufahamu karama ya imeinuliwa kukutana ukuta unaozuia kuingia ni upinzani utakaodumaza karama na huduma yako kwa hilo dumu ktk maomi Yesu akupiganie.

Ukiona unaendesha gari ktk maono ukiwa umelala ufahamu una huduma ya kanisa kubwa na namna unavyojitoa kutumikia mungu upo ktk njia ya uzima anayotaka na anakupeleka kwenye ukamilifu zaidi.

Ukiona nyumba ktk maono ukiwa umelala ufahamu Mungu ana mpango wa kukubariki kwenye wokovu wako ili ujenge nyumba.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ufahamu maono hayo ukachangake dumu ktk kuomba kwa kadri roho mtakatifu atavyokuongoza. Kwa kuwa Yesu amebadilisha utu wa ndani tangu uokoke.

## 10. MTU ANALIA KWA KUTAKA MSAADA;MIMBA;MAJI

Ukiona mtu analilia amesimama mbali nawe kidogo ktk maono ukiwa umelala fahamu mtu huyo amepatikana na mabaya au anawakilisha kundi la watu waliopatikana na mabaya utatuzi wa hao wasiendelee kupatikana na mabaya upo kwako.

Ufahamu watu hao wanahitaji maombi yako au wale wawatendeao mabaya adui zao wanahitaji maombi yako ili wabadilike. Kama mhubiri maana yake waombee waokoke watenda mabaya waokoke pengine ni watu walitakiwa wafikiwe na injili yako ili wasiwatende mabaya wenzao.

Ukiona maji yanamwagika ktk bomba hakuna chombo cha kuyakinga na Roho mtakatifu anakushudia hiyo ndiyo hali yako ya kiroho maana una upako usioutumia vizuri nguvu za mungu zinakutoka-bure karama ya imani imeinuliwa hufahamu namna ya kuitumia ,Chunga shauku yako ili hayo maji yaliyo hai yabubujikayo ndani yako yatumike vyema kama mhubiri kaa shauku ya kuona wenye dhambi wengi wakiokoka kupitia wewe kama mtu wa kimataifa uliyeoka bado ufahamu sana mambo ya huduma za kanisa tarajia mema tu kuza chochea karama ya imani iliyo ndani yako.

Ukiona mwanamke mwenye mimba aliyepitiliza miezi zaidi tisa ukashuhudiwa tatizo la linatoka uchawi ufahamu kama mtumishi wa Yesu atakutana na mwanamke huyo pengine amerudishwa nyumbani na hajazaa mimba anayo pengine haoni uchungu na utamwombea.

Ukiona upo mahali kama ndani ya nyumba ktk maono ukiwa umelala usiku na mbele yako unamwona mwanakondoo amechinjwa na damu yake inamwagika na roho mtakatifu akikushudia ni Yesu ufahamu Kama umeokoka ee mtu wa kimataifa jisikie huruma Yesu anataka uwahubirie wengine waokoke kama ulivyookoka wapate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na mungu. Ktk kazi yake mungu aliyokupa itahitaji damu ya mwanaye Yesu ili wenye dhambi waokokoke.

# 13. SAUTI YA MUNGU

Ukiona ktk maono umelala unashuhudiwa na roho mtakatifu kwa ishara izikilize roho yako unaisikia inakoroma sauti ya Mungu inasema mbona umelala ghafla ukaamka ufahamu kama ni mwombaji huombi sawa na mapenzi ya mungu ipo mbaya unakuja mbele hutaweza kuomba; pengine wewe si mwombaji na umeokoka badilika na uwe umwombaji; unafuatiliwa na kifo; umeingia majaribu kwa kutokuwa na maombi ya muda mrefu mfano maombi ya masaa 8 au 6 au 4.

**Yoh 11.11 – 14**

" Aliyasema hayo; kisha, baada ya hayo, akawaambia, Rafiki yetu, Lazaro, **amelala;** lakini ninakwenda nipate kumwamsha. ,Basi wale wanafunzi wakamwambia, Bwana, ikiwa **amelala,** atapona. Lakini Yesu alikuwa amenena habari ya mauti yake; nao walidhania ya kuwa ananena habari ya **kulala** usingizi. ,Basi hapo Yesu akawaambia waziwazi, Lazaro **amekufa.** "

**Marko 5:39 — 42**

"Alipokwisha kuingia, akawaambia, Mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana **hakufa,** bali **amelala** tu. Wakamcheka sana. Naye alipokwisha kuwatoa nje wote, akamtwaa babaye yule kijana na mamaye, na wale walio pamoja naye, akaingia ndani alimokuwamo yule kijana. Akamshika mkono kijana, akamwambia, Talitha, kumi; tafsiri yake, Msichana, nakuambia, Inuka. Mara akasimama yule kijana, akaenda; maana alikuwa amepata umri wa miaka kumi na miwili. Mara wakashangaa mshangao mkuu. "

**Mathayo 26.41 a**

"**Kesheni,** mwombe, msije mkaingia **majaribuni;** roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu. "

## 14. USHAURI KWA MAONO UNAOONESHWA MSAIDIZI

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka msaidizi wa unamfahamu au unamkumbuka ? Msaidizi wako ni **roho mtakatifu** na mojawapo ya usaidizi anakupa ktk wokovu wako ni kukupasha habari juu ya mambo ya baadaye yatokayo kwa Yesu na <u>**maono**</u> ni njia mojawapo anayoitumia roho mtakatifu kutoa usaidizi wake huo.

**Yoh 16.13**

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na **mambo yajayo** atawapasha habari yake. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka uliye kijana umejaa roho mtakatifu kupata maono kutoka kwa roho ni jambo la kawaida sehemu ya ko ya ndoto kabla hujaokoka imenunuliwa mungu kwa damu ya Yesu na inatumiwa roho mtakatifu kukupatia maono.

Maono yatokayo kwa roho mtakatifu ni ya kweli hilo alilokuonesha litatukia kweli au jambo uliloandaliwa na mungu lililo jema utalipata kweli.

Biblia inatumika kutafsiri maono yatokayo kwa Yesu. Ukipata maono kama huyaelewi omba roho mtakatifu akutafsirie kwa imani au akutafsirie kwa kutumia biblia akifundisha maana ya maono aliyokuonesha au aliokuonyesha. Ukikutafsia ukaelewa muulize mungu ufanye nini ili kama mema uyapate kama mabaya ukuepushe .

Ustajabie Yesu amebadilisha utu wako wa ndani baada ya kuokoka unaweza kuishi ktk wokovu baada ya muda fulani unaoneshwa jambo ukiwa umelala na unashuhudiwa ni Amina na kweli na Roho mtakatifu na likatukia mshukuru mungu kwa upatanisho maana mawasiliano kati yako nawe yamerejeshwa yale adamu mzazi wa mwanzo aliyapoteza kwa sababu ya dhambi.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or  0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034